# FUNGUO ZA BIBLIA

Tafadhari zingatia-, **kwakusoma biblia yako kwa kila andiko utakaloaneshwa katika kijitabu hiki.**

Leo tunaangazia somo la maandiko matakatifu katika Biblia na namna ya kujifunza na kuelewa.Biblia si kitabu laisi kukielewa kama wengi wanavyosema!, kiukweli ni vigumu mtu kukubali kwamba anaifahamu na kuielewa Biblia yote!.

**Ebu tuanzekujifunza leo na tuone NINI maana ya neno BIBLIA?**

Neno hili ni la **kigiriki = "Biblos"** maana yake ni **kitabu!.** Kitabu cha nini?, **Ni kitabu cha Mungu.**
**MUNGU ALIANDIKA KITABU AMBACHO NI NENO LAKE KWA WATU WOTE!**

Dunia inavitabu vingi sana vinavyoitwa **VITABU VITAKATIFU,** Kwa miungu ya dini mbalimbali. Vitabu vitakatifu vya dini ya **kihindu** vinaitwa **vedas** kama vile:- **Rig veda, Yajur veda, Sama veda** na **Atharva veda.** Lakini **Biblia** kwa lugha ya **kihindi** inafahamika kwa jina la **SATHYA VEDA** au **VEDA YA UKWELI.**

Kabla hatujaanza kujifunza kuhusu **Funguo za kufungua Biblia** na **kuelewa Biblia** acha tujifunze ukweli fulani na undani wake kuhusu kile kilichomo katika **Biblia.** Maandiko matakatifu yamegawanywa katika **Makundi Mawili** ambayo ni:-

1. **AGANO LA KALE**
2. **AGANO JIPYA**

Agano la kale lina jumla ya **vitabu 39** kwa Madhehebu mengine **lakini wakatoriki viko 46.**

Agano Jipya linajumla ya **vitabu 27**, kwahiyo jumla ya vitabu vyote ni **66** kwa wamadhehebu na **vitabu 72** kwa **kanisa katoriki.**

**Vitabu vitano(5)** vya kwanza katika Agano la kale vinaitwa **pentateuch** vilivyo andikwa na **musa.** Wayahudi **wanaviita TORAH** au **TORATI.** Ni vitabu muhumu sana kwao,kwani vimebeba **sheria** zilizowaongoza kutoka kwa mwenyezi Mungu!. **Biblia** imeandikwa kwa miaka isiyopungua **1700. Agano la kale ni miaka 1600** na **agano Jipya ni miaka 100.**

Hakuna kitabu kingine katika ulimwengu huu ambacho kinaweza kuchukua miaka mingi kuandikwa. **Je,**ni kitabu **kipi** cha kwanza kuandikwa katika Biblia?
**Kitabu cha Ayubu** ni cha kwanza na **kitabu cha ufunuo** ni cha mwisho kuandikwa **mwaka 96 BK.**

Watunzi **40** walitumiwa na **Mungu kama vyombo vyake kwaajili ya kuandika NENO LAKE.**

👉**LUKA-** alikuwa ni Daktari (**Wakolosai 4:14)**
👉**MATHAYO -** alikuwa Mtoza ushuru (**Luke 5:27,28)**
👉**DAUDI:-** alikuwa ni mchungaji na baadaye akawa mfalme(**1samueli 16:19)**
👉**SULEMANI:-** alikuwa mfalme(**1wafalme 2:12)**
👉**MUSA:-** alikuwa ni msomi alieandaliwa kuwa mrithi wa **Farao** mfalme wa **misri(kutoka 2:10)**
👉**PAULO:-** alikuwa ni mfarisayo(**Matendo 23:6)**
👉**AMOSI:-** alikuwa mchungaji maskini(**Amosi 7:14)**
👉**PETRO:-** alikuwa mvuvi kama YOHANA, na kadhalika na kadhalika(**Mathayo 4:18-21)**

**KITU CHA AJABU NA CHA KUSHANGAZA - ni kwamba Biblia ni kitabu kinacholeta AMANI na UPENDO pasipo mgongano wowote.**

👉**Kwahiyo tunaelewa kwamba Mtunzi sahihi wa Biblia ni Mungu Mwenyewe kwakutumia vyombo vya kibinadamu.**

Tunasoma na kuthibitisha jambo hili katika(**waebrania 1:1-2, 2Timotheo 3:16)**

“ ***Mungu,ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika mwana,aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu”***
***“ kila andiko, lenye pumzi ya mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwakuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki;”***

Kwahiyo tunaona kwamba katika vitabu vingi vya **Dunia** hii, Biblia ni kitabu ambacho kinasomwa zaidi hata na wale wasio **WAKRISTO** kwa **mfano, Mahatma Gandhi** na **Jawaharlal Nehru** pia **Dalai Lama.**

**👉AMINI USIAMINI!!**

Ukweli ni kwamba uhuru wa Taifa la **India** ulipatikana kupitia **Biblia!**
**Mahatma Gandhi** ni Baba wa taifa la india, na alipenda sana kusoma **Biblia,** na katika soma yake alikutana na **aya** ya **(Mathayo 5:39)**

“ ***Lakini mimi nawaambia,msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume,mgeuzie na la pili.”***

Hii ikapelekea kukoma kwa ualifu na maandamano ya **ahimsa** na **India** ikapata uhuru. Mpaka leo **aya** ya **(Mathayo 5:39)** inapatikana kwenye **Jengo la Bunge la Taifa la India.** Lakini watu wachache tu wanafahamu kwamba maandiko **haya** yanapatikana kwenye **Biblia,** lakini wengi **wanafahamu ni maneno ya Mahatma Gandhi!!**

Pia tunaona kwamba Biblia ni kitabu kilicho chapishwa mara nyingi zaidi ya vitabu vyote toka **mwaka 1454 Bk.** Kwa sasa Biblia imechapishwa **zaidi ya lugha 2000 ulimwenguni.** Lakini licha ya haya yote Biblia ni kitabu kinachowashinda wengi kukielewa kwa kugha **yake na alama zake.** Kinashindwa kueleweka hata kwa **idadi kubwa ya wakristo wenyewe!!**

**👉 NDIYO! BIBLIA NI CHAKULA CHA KIROHO TOKA KWA MUNGU KWA MWANADAMU!**

Ebu tusome**(Mathayo 4:4, Torati 8:3, Jeremia 15:16)**
Hii ni kama chakula asilia kinavyotofautiana virutubisho, hivyo ndivyo ilivyo katika **chakula cha kiroho.** Kivipi, unaweza kuuliza?

Tunasoma**(waebrania 5:12-14)**

**“*Kwa maana, iwapasapo kuwa walimu,(maana wakati mwingi umepita),mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu. Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwakuwa ni mtoto mchanga. Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima,ambao akili zao,kwakutumiwa,zimezoezwa kupambanua mema na mabaya.”***

**Ndiyo!,** hapa mtume paulo anaonesha **waziwazi** utofauti wa **chakula cha kiroho**

**👉MAZIWA na CHAKULA KIGUMU**

**Mtoto** anayekua anaanza na **maziwa** na baadaye **chakula kigumu.** Pia ni sawasawa na **kukua kiroho** lakini mtume paulo anasema wengi hawajakuwa **kiroho kabisa.**

**👉Nini maana ya Maziwa?**

**(waebrania 6:1-3, 1petro 2:2)**

***“Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa watamani maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu”.***

**Ndiyo!** Kukua **kiroho** ni lazima uanze na **maziwa** kama ilivyo katika makuzi ya **kimwili**

**Sasa**! Ebu tuje kwenye swala la msingi, **ni namna gani yatupasa kusoma Biblia Ili hali ni kitabu kigumu kukielewa!. Na inaonekana ni kitabu ambacho kimefungwa!**

👉**NI FUNGUO ZIPI HIZO ZA KUFUNGULIA BIBLIA?**

**Ndiyo!** Kwa neema za mwenyezi Mungu **leo tunaenda kuona funguo tatu (3) za dhahabu za kufungulia Biblia.**

🔑 **UFUNGUO WA DHAHABU WA KWANZA.**

**(Isaya 28:10)**

***"Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri,kanuni juu ya kanuni,huku kidogo na huku kidogo"***

**Je,**umeelewa nini **aya hii** inamaanisha?

**Sawa!,**jibu lililozoeleka ni **HAPANA!.** Ni vizuri kuelewa **aya** tunayoizungumzia kama ilivyoonekana hapo juu.

**Ndiyo!,** cha msingi ni kujifunza na kuelewa mafundisho(maandiko matakatifu) ya Biblia.

**Katika funguo ya kwanza ya dhahabu -** aya ya kujifunza maandiko matakatifu ni palipo andikwa:-

"**.... amri juu ya amri....**
**sheria juu ya sheria"**

Hii inamaanisha nini?

**Hapa neno** "AMRI" linamaanisha .... **Mafunzo** au **masomo,** na **neno** (SHERIA) lina maana... ya **aya.** Inabidi kuwe na mfumo maalumu au utaratibu maalum wa kujifunza masomo au katika mafunzo na masomo yenyewe yawe na mpangilio wa **aya(sheria),** Lakini zingatia kipengele cha mwisho kilichoandikwa

***" ....huku kidogo na huku kidogo"***

Hii inamaanisha

👉**AYA ZINAZOTAKIWA KUJIFUNZA ZIMEENEA KATIKA BIBLIA KAMA ZILIVYO...**

***"... huku kidogo na huku kidogo"***

Hii inamaanisha nini?

Acha tuangalie **mfano, je, unajua Biblia inaongelea mtu ambaye hakuweza kufa?**

**Ndiyo!,** jina lake...**ENOKI.** Storia hii ya **ENOKI** katika Biblia inapatikana katika **aya tatu(3) tu,** na zote hizo zimetapakaa katika Biblia nzima. Andiko la kwanza tunalipata katika kitabu cha**(mwanzo 5:24, waebrania 11:5 na Yuda 14)**

Kwahiyo hii ndiyo **kanuni** ya **"*huku kidogo na huku kidogo*"**

Tena **kwanini** imetajwa **tena na tena(mara mbili)**

***"...amri juu ya amri,amri juu ya amri;***

Kama tulivyoona katika neno **amri** linamaanisha **mafunzo au masomo,** na neno **sheria** linamaanisha ni **aya.** Kitendo cha kurudia jambo marambili inamaanisha **ukweli kwamba MAFUNZO YOTE YA BIBLIA YAPASWA KUGAWANYWA KATIKA SEHEMU KUU MBILI YA NENO LA MUNGU,** Yaani:-

👉**Agano la kale na Agano jipya**

**Hivyo,** kwanini **aya.... " *huku kidogo huku kidogo*"** katika Biblia?

Tunasoma kuhusu jambo hili katika**(Isaya 34:17)**

***"Naye amewapigia kura, na mkono wake umewagawanyia kwa kamba; wataimiliki hata milele,watakaa ndani yake kizazi hata kizazi"***

Hapa neno **kura** linaonekana kama neno geni kulielewa!

### 👉NI KWA NAMNA GANI MUNGU AMETUPIGIA KURA KUDHIHILISHA UKWELI WAKE?

**Vizuri!** Katika zoezi la kupiga **kura** kipande kimoja cha **karatasi** ambacho kimechanwa chanwa vipande vipande na katika kila kipande kimeandikwa jina la kila mtu wa kupigiwa **kura!**

Hii ni sawa kabisa katika maandiko matakatifu ya **Mungu** na **Mafundisho** yenye **ukweli,** yamegawanyika katika **vipande** au **aya.**

**Ndiyo!** Mungu mwenyewe amegawanya **ukweli mstari kwa mstari** ambayo ni **aya** na pia Mungu kazichukua **aya** zenye mafunzo **yenye mficho au mafumbo na kuzitawanya katika vitabu vyote 66 au 72 vya Biblia.**

### 👉HUU NI MFUMO WA KIMUNGU WA KUFUNGA UKWELI!

**Kwanini Mungu amefunga ukweli?**

Hii ni kwakuwa **ukweli huo ni wenye thamani kubwa ili usiweze kudharaulika na kutumiwa vibaya.**

Tazama binadamu anahifadhi vitu vyake vya thamani na kufunga kwa **kufuri** kwaajili ya usalama, wakati mwingine hufungia vitu vyake vya thamani kwenye **masanduku mbalimbali** yanayofungwa kwa **namba.**

**Je,**ukweli wa **Mungu unathamani gani?**

Tunaona Biblia imefungwa **Je, tunaifunguaje!** Jibu tunapata katika**( Isaya 34:16)**

***"Tafuteni katika kitabu cha Bwana mkasome; hapana katika hao wote atakayekosa kuwapo, hapana mmoja atakayemkosa mwenzake; kwa maana kinywa changu kimeamuru,na roho yake imewakusanya"***

**Ndiyo!,** hapa tunaona kwamba mtu anahitaji kutafuta kiundani neno la Mungu katika **aya** zote.

### 👉kila aya ina jozi yake.

Nini maana ya **jozi?**

**Mfano, mke na mume** ni **jozi** moja, pia hata nyaya za umeme ziko katika jozi, kuna nyanya **hasi** na **chanya** zote ziko katika jozi . Hivyo basi, kila **aya** yenye Swali ina oana na **aya** yenye Jibu!.

**Ndiyo!,** kunajibu kwa kila **swali** katika Biblia!. Lakini mtu anahitaji **Roho ya Mungu** kuweza kukusanya au kutafuta hayo yote kwa mpangilio maalum**(Yohana 16:13).** Hivyo, kunahitajika **mafunzo yenye mpangalio maalum** wa masomo,pia **aya** za kujifunzia zote zilizotawanyika katika **vitabu** 66 au 72 katika Biblia. Kabla hatujaenda kwenye **UFUNGUO 2 WA DHAHABU** ni namna gani tijifunze **Biblia?**

Ebu tujifunze jambo moja muhimu na **maana yake (Isaya 28:10,13)**

"***Kwa maana ni amri juu ya amri,amri juu ya amri;kanuni juu ya kanuni,kanuni juu ya kanuni,huku kidogo na huku kidogo. Kwasababu hiyo neno la BWANA kwao litakuwa hivi,amri juu ya amri,amri juu ya amri;kanuni juu ya kanuni,kanuni juu ya kanuni;huku kidogo na huku kidogo;ili waende na kuanguka nyuma,na kuvunjwa,na kunaswa,na kuchukuliwa***"

Tazama mfanano wa lugha na bado kuna utofauti mkubwa katika **aya** hizi 2!

**Je,zinamaanisha nini?**

### 👉Zinaongelea kuhusu ... masomo mawili ya Biblia.

Kwakuwa tumeshasoma kabla(**Isaya 28:10).** Somo au funzo hili la **Biblia** linakupeleka mbele ili kujua au kupata ufahamu wa **ukweli.** Pia tena soma **aya(Isaya 23:13)**

"***Tazama,nchi ya wakaldayo;watu hao hawako tena;Mwashuri ameiweka tayari kwa hayawani wa jangwani;wamesimamisha buruji zao za vita,wameyaharibu majumba yake ya enzi,akaufanya kuwa uharibifu***"

**Je,inamaanisha nini?**

Somo au funzo hili la Biblia **linakuludisha nyuma katika ufahamu au kichocheo 1 cha kupoteza UKWELI!**

Na tazama lugha iliyotumika na maana yake!

“***....na kuvunjwa,na kunaswa,na kuchukuliwa***”

Inamaanisha…. **Kukamatwa na maandiko ya uongo na yenye makosa ya kutodhihilisha ukweli!**

👉**Hapa ndipo swali linapoibuka - NI NAMNA GANI TUTAJUA HUU NI UKWELI?**

Tunapata jibu katika**(Yohana 17:17)**

“***..... Neno ni ukweli”***

Je, mtu atatambuaje umuhimu wa jambo hili?

👉**HILI NDILO SOMO SAHIHI LA KUJIFUNZA!!**

**Ndiyo!-** kwa zoezi la kuamini kile kilichofundishwa! **Ndiyo, kuna mafundisho ambayo yanaendana na maandiko matakatifu?**

Ebu tufanye zoezi kutoka katika maandiko matakatifu

**JE, ROHO INAWEZA KUFA JEHANAMU(MOTONI)?**

Wengi watajibu **hapana!.** Lakini tunafundishwa kwamba **roho yaweza kufa motoni!**

Kwanini!!!? **Kwasababu tunasoma hili katika maandiko matakatifu (Mathayo 10:28)**

“***Msiwaogope wauao mwili,wasiweze kuiua na roho;afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanam.***”

Umeona hiyo???! **Biblia inatufundisha hivyo….**

**ROHO INAWEZA KUANGAMIZWA MOTONI NA PIA HATA MWILI UNAENDA MOTONI!**

**Je, umefurahi???**

**Aah!** Tutajifunza kiundani kuhusu **roho ya binadamu** katika madarasa ya mbele! Kwahiyo, mara zote jaribu iwapo yote **unayojifunza** katika **Darasa la Biblia** linamsingi wa maandiko matakatifu na kuna **aya** ambayo inathibitisha **imani hiyo kwakuwa Biblia yenyewe inaonya kuhusu …. MAFUNDISHO YA UONGO NA MAFUNZO YA UONGO YASIYO YA KIBIBLIA.**

Sasa,**ebu tujifunze** 🔑**UFUNGUO WA 2 katika kujifunza Biblia** **(2Timotheo2:5)**

“***.Hata mtu akishindana katika mchezo hapewi taji,asiposhindana kwa halali.***”

**Je,** inamaanisha nini? **Hapa kuna siri kubwa!** Tunafahamu kwamba katika **lugha** nyingi za binadamu zina mfumo wake au **muundo wake,**

**Kama vile:-** MASHAIRI, RIWAYA,TENZI na kadhalika. **Inabidi tuwe waangalifu …. Kutambua muundo wa lugha iliyotumika katika maandiko matakatifu.**

**Ebu,** tutazame **miundo** ya lugha iliyotumika katika **Biblia**

1. **Lugha ya Wazi wazi ( Lugha nyepesi )**

**Kwa mfano,** lugha ya wazi wazi ni kama katika kitabu cha **(Mwanzo 1:1, Mathayo 1:21)**

“***Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi.***”

“***Naye atazaa mwana,nawe utamwita jina lake Yesu,maana,yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.”***

Katika sehemu kubwa ya Biblia imeandikwa kwa **lugha nyepesi kuelewa.** Haina ugumu wowote katika kuelewa. Lakini tukumbuke kwamba katika **Biblia hiyo hiyo** kuna baadhi ya vitabu havijaandikwa kwa lugha ya wazi wazi.

**2 .Lugha ya mafumbo**

Lugha hii imeoneshwa katika **sura na aya kadhaa** katika Biblia. Sura hizo hazija andikwa kwa lugha ya wazi wazi **lakini kiroho zaidi.** Ebu tuchunguze **mfano wa lugha ya mafumbo ili kuweza kuelewa zaidi jambo hili.**

Tusome katika kitabu cha **(Luka 15:3-7)**

**"*Akawaambia mfano huu,akisema,ni nani kwenu,mwenye kondoo mia,akipotewa na mmojawapo,asiyewaacha wale tisini nakenda nyikani,aende akamtafute yule aliyepotea hata amwone?. Naye akiisha kumwona,humweka mabegani pake akifurahi. Na afikapo nyumbani kwake,huwaita rafiki zake na jirani zake,akawaambia, Furahini pamoja nami,kwakuwa nimekwisha kumpata kondoo wangu aliyepotea. Nawaambia,vivyohivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwaajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye,kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja ya kutubu.*"**

**Aah ndiyo!** Hili ni fumbo ambalo tumelizoea kwakuwa linasomwa **mara kwa mara Katika sakramenti ya UBATIZO,**

Pale wakristo **wapya wanapobatizwa..** Wengi wanafikiri kwamba **aya ya 7 inamaanisha MDHAMBI MMOJA TU , KWAKUTUBU NA KUMRUDIA MUUMBA WAKE.**

Lakini ebu chunguza kwa makini **aya hii 7**

**"*Nawaambia,vivyo hivyo kutakuwa na furana mbinguni kwaajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye,kuliko kwaajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja ya kutubu.*"**

**kama kweli inamaanisha MDHAMBI MMOJA.**

**Sasa je, hawa 99 wanaozungumziwa hapa ni wakina nani?.**

**Je, kuna wenye haki wengi sana katika hii Dunia?**

**Jibu la swali hili linapatikana katika**

**(Warumi 3:10)**

**"*Kama ilivyoandikwa,ya kwamba,hakuna mwenye haki hata mmoja.*"**

**Hili** ni fumbo ambalo halimaanishi **mdhambi mmoja tu.** Acha sasa tuone maana yake.

**Yesu hapa anaongelea mtu aliye na kondoo 100.** Utajiri wa wakati huo ulikuwa unahesabiwa kwa idadi ya kondoo,ng'ombe,ngamia na kadhalika. **Mfano, Abraham,Ayubu n.k**

**Ambaye pia anajulikana kwa jina la MCHUNGAJI(Zaburi 23:1)**

***"Bwana ndiye mchungaji wangu,sitapungukiwa na kitu."***

**KONDOO WA MUNGU NI WEPI?**

**100**- inamaanisha aina ya viumbe vyote vilivyoumbwa. 100 ni namba ya makadilio ya viumbe vyote vilivyoumbwa, ijapokuwa uumbaji wenyewe unajumuisha zaidi ya 100 kati ya vilivyoumbwa.

**Kondoo**- Inamaanisha ni viumbe vitiifu kwa mwenyezi **Mungu.** Kondoo mmoja wa aina moja au aina moja tu ya kiumbe ndicho kilichopotea.

**Kiumbe hicho ni BINADAMU!.** Binadamu akipotea kwakutenda dhambi na mshahara wake ni kifo**(Warumi 6:23)**

**"*Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya mungu ni uzima wa milele katika kristo yesu Bwana wetu."***

***Je,***Mungu alifanya nini?

**Ndiyo,** alimtumia mwanae wa pekee kwakuwatafuta KONDOO waliopotea**(yohana 3:16)**

**Ndiyo,** tutajifunza katika madarasa ya mbele kuhusu **mpango wa mwenyezi Mungu katika ukombozi wa binadamu wote.**

**Ndiyo, na mwisho kutakuwa na furaha kubwa mbinguni wakati binadamu atakapokombolewa kutoka katika utumwa wa dhambi ya mauti, na kupata tumaini la uzima wa milele.**
Kuna mambo mengi ya kuyaelewa katika fumbo hili zaidi tutajifunza kiundani katika madarasa yafuatayo. Lakini huu ni mfano wa kuelewa lugha ya mafumbo..!!

### 3. Lugha ya alama

Hii ni lugha ambayo alama zimetumika kificha maana ya **unabii mkubwa n.k.** kitabu cha **ufunuo** ni kitabu kizima kilichojaa **alama** kama tunavyosoma katika**(Ufunuo 1:1)**

***"Ufunuo wa yesu kristo aliopewa na mungu awaoneshe watumwa wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi,naye akatuma kwa mkono wa malaika akamwonesha mtumwa wake yohana;)***

Pia lugha hii inaonekana katika vitabu kadhaa vya Biblia kama vile **Ezekieli,Danieli n.k.**

Alama kwa **asili** zinazotuzunguka ni kama vile
**upepo,maji,miinuko,milima,miji,mawingu,miti,nyasi,pembe,moto, n.k.** utumika na kila moja inatoa maana yake mojo kwa moja katika **Biblia**
yenyewe!

**Ebu tuangalie mfano katika( Mathayo 16:6) ina maana gani?.Acha tusome jibu katika(Mathayo 16:12)**

***"Ndipo walipofahamu yakuwa hakuwaambia kijilinda na chachu ya mkate,bali na mafundisho ya mafarisayo na masadukayo."***

**Ndiyo!** Mafundisho ya mafarisayo na masadukayo yalikuwa MAFUNDISHO YA UONGO kama tunavyosoma**(Matendo 23:8)**

**"*Kwamaana masadukayo husema ya kwamba hakuna kiyama wala malaika wa roho;bali mafarisayo hukiri yote"***

**Ndiyo! Ivyo kama mungu anavyotuambia- kama alama ya mafundisho ya UONGO.**
Acha sasa tusome **aya** nzima yenye lugha ya **alama** katika **(Mhubiri 11:1)**

**"*Tupa chakula chako usoni pa maji maana utakiona baada ya siku nyingi."***

**Je,**hii itachukuliwa kama lugha ya waziwazi?. Kama unaweka mkate kwenye maji, utayeyuka kwa mda mfupi,na kutoacha mabaki yoyote!. Kwahiyo **utawezaje kuupata?**
**"*..... baada ya siku nyingi"?***

**Aah! Ndiyo,** hii ni lugha ya **alama**!!

**Ebu tujifunze alama TATU (3) zilizotumika na maana zake ni:-**

**1.Mkate - ni** NENO LA MUNGU**(mkate wa kiroho Yeremia 15:16, Mathayo 4:4)**
**2. Maji- ni ULIMWENGU wa watu, makundi,nchi, na ndimi, kama tunavyosoma katika ( Ufunuo 17:15)**
**3. Baada ya miaka mingi-** ni **muda wa utawala wa MWENYEZI MUNGU HAPA DUNIANI ambapo tunasoma jambo hili yakuwa watu wote watubu na kumgeukia Mwenyezi Mungu kama tunavyosoma katika (Zaburi 22:27-28)**

***"Miisho ya dunia itakumbuka,na watu watamrejea ,Bwana;jamaa zote za mataifa watamsujudia,maana ufalme una Bwana,naye ndiye awatawalaye mataifa."***

**Je,** umeona hiyo?! **Ivyo** Aya hii inaongelea **USHAHIDI wa ukweli** sasa kabla watu hawajategemea sasa bali **ni** kwa wakati ujao.

**HIVI NI SAHIHI KWAMBA MTU ANAWEZA KUUGAWANYA UKWELI au KUSAHIHISHA NA KUELEWA MUUNDO WA LUGHA ILIYOTUMIKA ILIKUPATA UKWELI?!**

Kama lugha ya **alama imetumika** mtu haimpasi kuchukulia hiyo kama ni **lugha ya waziwazi** na pale lugha ya waziwazi inapotumika **mtu** haimpasi kuchukulia hiyo kama ni **lugha ya mafumbo au vinginevyo.**

Sasa ebu tuje katika 🔑 **FUNGUO YA TATU (3) KATIKA KUJIFUNZA BIBLIA.**

Katika funguo ya 3 kwa masomo ya Biblia ni **vema kujua jumla ya mada za kujifunza kwakutafuta AYA kwa masomo yote katika Biblia.**

***"…..huku kidogo na huku kidogo"***

Kwamfano, somo la **ROHO,UKOMBOZI,UBATIZO,KANISA n.k** utashangaa namna **Maandiko matakatifu yanavyoendana na MADA maalum** yafaa kuoneshwa na kufikiriwa.

**HII NI SHUGHULI KUBWA! lakini baraka za Mungu zitasaidia katika jambo hili kwa wale waliojitoa KWAKE.**

Ndiyo! Kwa msaada wa kutafuta **aya mbalimbali** katika somo husika kwa mfatano wa **aya zote zilizo kuwemo na zinazooana katika mada mbalimbali.** Katika Biblia vitu 2 vinavyoendana vimeandikwa na **wenye lika tofauti tofauti** vijana na wazee.

**Ivyo,** kwakusoma Biblia kutoka katika kitabu cha **mwanzo hadi ufunuo sura kwa sura, aya kwa aya haitakusaidia kuupata UKWELI sahihi kabisa kutokana na utofauti wa lugha zilizotumika.**

***".....huku kidogo na huku kidogo"***

**Ivyo basi! Kwakufuata utaratibu huu ambao una matunda na wenye neema katika kusoma masoma mbalimbali yaliyomo katika Biblia,kwakutambua miundo na mitindo ya lugha zilizotumika unaweza kuupata ukweli sahihi**

**Je,umeelewa FUNGUO HIZI 3 KATIKA UJIFUNZAJI WA BIBLIA, ebu tuhitimishe kwakujifunza mifano ifuatayo:-**

**KWANINI NENO LA MUNGU LIMECHORWA/KUFANANISHWA KAMA "MOTO" NA "NYUNDO"? (Yeremia 23:29)**

***"Je! Neno langu si kama moto? Asema Bwana;na kama nyundo ivunjayo mawe vipande vipande?"***

**Ndiyo!** Hapa Mungu amefananisha **moto** na **nyundo. Je,anamaanisha nini?!**

**MOTO**- ni alama ambayo kwayo inaharibu na kusafisha!!. Katika maisha ya kila siku ya mwanadamu **moto huaribu na kusafisha/kuteketeza takataka.**

**Pia** neno la **Mungu ni kama moto kwani LINAHARIBU DHAMBI NA KUSAFISHA MOYO KATIKA KILA AINA YA DHAMBI NA UCHAFU**

**NYUNDO**- Hapa inamaanisha kama **jiwe kubwa imara. Nyundo inatumika kuvunjia mawe makubwa!**

**Ivyo! Neno la Mungu ni KAMA NYUNDO KUBWA AMBAYO INAVUNJA NA KUACHA MOYO ULIO MGUMU KATIKA DHAMBI NA UBINAFSI KUWA HURU.**

Tena tunasoma **alama** ya **Mwanga(Zaburi 119:105)**

**Ndiyo!** Hapa neno la Mungu limechorwa kama **mwanga. Je, nini maana yake?** Ili kuelewa **alama** vizuri inatupasa kusoma katika kitabu cha**(Isaya 60:2)**

***"Maana, tazama,giza litaifunika dunia,na giza kuu litaifunika kabila za watu,Bali Bwana atakuzukia wewe,na utukufu wake utaonekana juu yako"***

**Ndiyo!** Hii si lugha ya waziwazi **Giza** lakini **alama ya Giza!** Dunia nzima na watu wake imeandikwa itafunikwa kwa **giza**. Maana ya **giza** imeeleweka wakati tulipoona **alama ya Mwanga.**

**Ndiyo! Mwanga wa neno la Mungu ni UKWELI (Yohana 17:17).**

**Giza**- linamaanisha **UONGO au ISIYO YA KWELI.**

**Neno la Mungu ni UKWELI(MWANGA) katika ulimwengu wenye GIZA(pale penye UONGO)**

**Pia,** tunasoma **alama nyingine ambayo ni UPANGA(Waefeso 6:17)**

***"Tena ipokeeni chepeo ya wokovu,na upanga wa roho ambao ni neno la Mungu"***

**Ndiyo!** Hapa ulimwengu umechorwa kama **upanga!**

**Upanga ni silaha ya kujilinda. Lakini hapa upanga UNAMAANISHA KIROHO. Ndiyo! Neno la Mungu ni SILAHA ya kiroho kujirinda dhidi ya UBAYA,UOVU kama tunavyosoma katika (Waebrania 4:12)**

***"Maana neno la Mungu lina uhai tena lina nguvu,tena linaukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili,tena lachoma hatakuzigawanya nafsi na roho,na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake,tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudio ya moyo."***

**Makali ya upanga** ni **alama ya neno la Mungu linavyoathiri WASIKILIZAJI NA WAONGEAJI.**

**Mwisho,** tunasoma **alama nyingine** ya **CHAKULA**.**(Torati 8:3)**

***"Akakutweza,akakuacha uone njaa,akakulisha kwa mana,usiyoijua wewe wala Baba zako hawakuijua;apate kukujulisha ya kuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu,bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha Bwana"***

**Hapa,** neno la Mungu limechorwa kama **chakula! Ndiyo!** Hii inamaanisha kama **chakula cha kiroho** kwa makuzi na maisha ya binadamu kadili anavyoendelea kuelewa ili kuweza kupata **uzima wa milele.**

**Mwisho kabisa tunasoma kitabu cha (2Timotheo 3:16,17)**

***"Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho,na kwakuonya watu makosa yao,na kwakuwaongoza,na kwakuwaadabisha katika haki. Ili mtu wa Mungu awe kamili,amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema"***

**Ndiyo! Njia bora ni kufahamu ukweli wote ili kumtumikia MUNGU kwa usahihi. Na ni muhimu kuwa makini katika maandiko matakatifu kwani haipaswi kuongeza neno au kupunguza neno litokalo katika kinywa cha MUNGU.**

**----------AMINA------------**



Imeandaliwa na Mwl
Bernardo Jordan Komba,
bernardokomba.bk@gmail.com,
+255763043486/255622361287.